BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA WA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Saba – Tarehe 01 Disemba, 2016.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mheshimiwa Mohammed Said Mohammed.

Hoja ya Mjumbe kuhusu Matokeo hatarishi katika Sekta ya Uwekezaji wa Viwanda nchini.

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

135. MHESHIMIWA SAID OMAR SAID (Jimbo la Wingwi):- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Katika hali ya ubora na upatikanaji wa haki kwenye Ofisi ya Muendesha Mashtaka, Idara hii ndiyo yenye mamlaka ya kuamua kuwa kesi fulani ipelekwe Mahakamani au la.

Kwa kuzingatia kuwa Wananchi wanajua chombo cha kutoa haki ni Mahakama na Hakimu ndiye mwenye

uwezo wa kutoa haki je, kitendo cha kuweka chombo chenye uwezo wa kuzuia dai au kesi kutofikishwa Mahakamani ni hali ya Utawala Bora.

Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

121. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Zanzibar ina misitu mikubwa ambayo kwa Unguja ni JOZANI na kwa Pemba ni NGEZI, na misitu hiyo imekuwa na vivutio mbali mbali kama vile, wanyama wa aina tofauti, makaburi ya zamani na ya asili ya maimamu, lakini kwa bahati mbaya vivutio hivyo havitangazwi kwa wageni na hata wenyeji wa Zanzibar.

a) Je, Misitu ya JOZANI na NGEZI ina vivutio vya aina ngapi na ni vivutio gani.

b) Je, serikali ina mpango gani wa kuwapandikiza wanyama waliomo kwenye misitu hiyo ili kuwaenzi na kueka hadhari ya kupotea kwa rasilimali hiyo ama kwa maradhi au matatizo mengine.

c) Je, Serikali inafaidika na mapato yanayotokana na makaburi hayo.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

79. MHESHIMIWA DKT. MAKAME ALI Ussi (Jimbo la Mtopepo) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Uwepo wa walimu wa Sayansi ni muhimu sana na naipongeza Wizara kwa kufanya bidii za makusudi za kutatua tatizo la upungufu wa walimu hao katika skuli zetu. Hata hivyo hivi sasa kuna upungufu mkubwa wa walimu wa masomo ya Art katika skuli mbali mbali.

Na kwa kuwa katika skuli za Jimbo la Mtopepo hasa skuli ya Mtopepo na Kidatu juu, kuna upungufu mkubwa wa walimu hao wakati wapo vijana wengi waliomaliza masomo yao ya ualimu kwa viwango vya Shahada, Stashahada na Cheti ambao hawajaajiriwa.

a) Je, kuna mpango gani uliopangwa kwa lengo la kutatua tatizo hili katika skuli zetu.

b) Wizara ina mpango gani wa kuwaajiri vijana hao ili wazibe pengo la upungufu wa walimu katika skuli za Jimbo la Mtopepo.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

114. MHESHIMIWA VIWE KHAMIS ABDALLA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Tatizo la mabibi shamba na mabwana shamba limechukuwa muda na tukiangalia tuna vijana ambao wameshasomea fani au taaluma hii, lakini mpaka leo hii vijana hao hawajapatiwa ajira.

Je, Mhe. Waziri Wizara yako ina mpango gani wa kuwaajiri vijana hawa ili kuondosha kero ambazo zinawafika wakulima wetu.

131. MHESHIMIWA SHAIB SAID ALI (Jimbo la Chonga) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Bonde la mlemele liliopo Jimbo la Chonga na Chambani limo katika mpango wa kilimo cha umwagiliaji zaidi ya miaka 10 sasa, lakini hadi leo hii hakuna hatuwa inayoendelezwa kutoka bonde hilo.

a) Je, kuna mpango gani wa kuliendeleza bonde hili ili wananchi wapate mavuno mazuri.

b) Je, ni sababu gani zilizopelekea bonde hilo lisiendelezwe hadi leo.

Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira :

133. MHESHIMIWA SHAIB SAID ALI (Jimbo la Chonga) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Moja kati ya uchafuzi na uharibifu kwa mazingira ni uchimbaji wa mawe, mchanga na ukataji wa miti ovyo, suala ambalo limejitokeza sana katika ukanda wa pwani wa mashariki ya kisiwa cha Pemba.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi hao ili wasiendelee kuchafua na kuharibu mazingira bila ya kuwaathiri wanachi hao kimaisha.

52. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Kwa kuwa Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwenye majibu wakati wa Bajeti alithibitisha kwamba Mwekezaji anaeitwa Mpapindi amefutiwa hati kumiliki wa eneo, lakini hadi leo hii mtu huyo yupo na anaendelea kuishi kwenye eneo ambalo hati yake imeshafutwa.

a) Je, ni kwa sababu gani mtu huyo anaendelea kuishi hapo na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa dhidi yake.

b) Je, ni lini Serikali itatoa amri ya kumuondoa eneo hilo kwa sababu hati yake imeshafutwa.

c) Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti mali yake ili kufidia deni la zaidi ya dola 4 milioni analodaiwa na Serikali kwa ajili ya kodi ambayo bado hajalipa kama ilivyoainishwa na Serikali.

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

120. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Serikali imeamuwa biashara nyingi kuwapa wafanyabiashara binafsi ili wawe ndio waendeshaji.

a) Je, Serikali ilifanya utafiti wa kina kuangalia athari za maamuzi hayo kimapato na kiusalama.

b) Je, kwa nini Serikali imekaa na kusubiri mapato kutoka kwa walipa kodi na kuacha vyanzo vya mapato ya kibiashara hasa kwa zile biashara ambazo zinawahusu wananchi moja kwa moja.

c) Je, Serikali imejipanga vipi kuziba pengo hili kabla ya kutokea madhara.

Wizara ya Afya

83. MHESHIMIWA MASOUD ABRAHMAN MASOUD (Jimbo la Bububu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya.

Sekta ya afya ni miongoni mwa sekta nyeti ambayo inahitaji uimarishaji wa hali ya juu. Hospitali iliyoko katika Shehia ya Mbuzini ni Hospitali ambayo jengo lake lilikuwa likimilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi kwa wakati huo ambapo kwa sasa ni Manispaa ya Magharibi (A). Jengo hilo lilimilikishwa kwa Wizara ya Afya kwa makubaliano ya kurejesha shilingi milioni 70 kwa Halmashauri husika.

a) Je fedha hizo zimeshalipwa na kama hazijalipwa zitalipwa lini.

b) Hospitali hiyo katika awamu iliyopita ilitembelewa na Mhe. Rais ambapo aliahidi kuwa Serikali itasimamia umalizaji wa jengo hilo ili kuifanya Hospitali hiyo kuwa ya Wilaya, Je, ahadi hiyo ya Mhe. Rais itatekelezwa lini.

147. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya.

Kwa kuwa Wabunge na Wawakilishi tumejitahidi sana katika majimbo yetu kununua gari za Wagonjwa (Ambulance).

Je, Wizara ina mpango gani wa kuzigawia mafuta gari hizo.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

55. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Serikali haijawa na mpango wa kuimarisha miundombinu ya bandari kwa upande wa Pemba ili meli za mizigo ziweze kufunga gati moja kwa moja katika bandari ya Mkoani na kushusha mizigo ikiwemo vyakula badala ya kushusha Unguja na baadae kusafirisha mpaka Pemba na kusababisha mfumuko mkubwa wa bei za bidhaa kwa kufidia gharama za usafirishaji.

a) Je, kwa kuwa tatizo hilo ni la muda mrefu na wanaoumia ni wananchi, Serikali italipatia lini ufumbuzi tatizo hilo ili kuwapa unafuu wa bei na upatikanaji wa mahitaji kama wanavyonufaika watu waliopo Unguja.

b) Kwa kuwa bandari ya Wete na Mkoani zinashindwa kufunga meli kubwa kuanzia tani 2000 za mizigo na kuendelea kutokana na kina chake cha maji kuwa kidogo, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kina cha maji na kufanya bandari ya kisasa kama ilivyofanyika bandari ya Malindi Unguja.

69. MHESHIMIWA SHEHE HAMAD MATTAR (Jimbo la Mgogoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji

Kwa kuwa Shirika la Bandari lina wafanyakazi waliogawiwa katika makundi mawili ambayo ni kundi ‘A’ na kundi ‘C’ ambapo kundi ‘A’ ndio lenye wafanyakazi wa kudumu na wanapata stahiki zote kama vile mishahara, likizo na mafao mbali mbali na kundi ‘C’ ndio lenye wafanyakazi vibarua ambao wengine wanafika takriban miaka 20 na hawajaajiriwa rasmi.

a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuwapatia ajira ya kudumu wafanyakazi hawa wa kundi ‘C’ ambapo wameshafanya kazi kwa muda mrefu ili

kutoa motisha wa kazi kwa wafanyakazi wengine wa kundi hilo.

b) Je, Wizara inafahamu kuwa wafanyakazi hawa wanafanya kazi katika mazingira ambapo hata vitendea kazi huwa hawapatiwi na wanapoumia katika kazi huwa wanajitibu wenyewe.

III. UCHAGUZI WA NAFASI ZA UONGOZI KWENYE UMOJA WA MABUNGE YA NCHI ZA JUMUIYA YA MADOLA TAWI LA ZANZIBAR.
HOJA YA MJUMBE:

Uchaguzi wa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati Tendaji na Mweka Hazina wa Umoja wa Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola Tawi la Zanzibar.

IV. HOJA YA MJUMBE:

Mheshimiwa Mohammed Said Mohammed.

Hoja ya Mjumbe kuhusu Matokeo hatarishi katika Sekta ya Uwekezaji wa Viwanda nchini.

Zanzibar,
01 Disemba, 2016.

(Amour M. Amour)
KNY. KATIBU